# MFUMO WA KUPUNGUZA TAKA

SKANI HAPA KWA
MIONGOZO KAMILI YA KUPUNGUZA

## MUONGOZO WA MAAMUZI YA KUPUNGUZA

**1. ONDOA** — Je, tunahitaji bidhaa hii?
HAPANA → **1. ONDOA**: Hatua yenye matokeo makubwa zaidi. Kama bidhaa hazihitajiki, ni kuondowa kabisa.
NDIYO ↓

**2. PUNGUZA** — Je, tunaweza kupunguza matumizi yake?
NDIYO → **2. PUNGUZA**: Tumia vifungashio vichache, eka sera za hiari, na epuka kutoa bidhaa au vifaa visivyohitajika.
HAPANA ↓

**3. BADILISHA** — Je, kuna chaguo bora zaidi?
NDIYO → **3. BADILISHA**: Badilisha plastiki zinazotumika mara moja, kwa plastiki zinazodumu, zinazoweza kutumika tena, au vinazooza kiasili.
HAPANA ↓

**4. CHAKATA** — Je tunaweza kuchakata tena kile kilichobaki?
NDIYO → **4. CHAKATA**: Hatua ya mwisho kwa taka zisizoepukika ambazo haziwezi kuondolewa au kutumika tena.
HAPANA ↓

**HAKUNA CHAGUO ZURI?** Fikiria ubunifu, utetezi, au mabadiliko ya mfumo.

**Usimamizi wa taka ni mojawapo ya changamoto kubwa zinazoikabili sekta ya utalii Zanzibar.**

Mfumo wa REDUCE unahamasisha shughuli za sekta ya hoteli na utalii kuondokana utamaduni wa "kutupa" hadi mfumo endelevu na wa uchumi mzunguko. Inaweka kipaumbele katika hatua za kuzuia taka katika chanzo chake, badala ya kutegemea zaidi hatua za usimamizi wa taka zinazofanyika baada ya uzalishaji.

Makundi matatu ya kipaumbele kwa hatua za haraka chini ya Miongozo ya REDUCE:

1. Chupa za plastiki za maji na vinywaji baridi.
2. Vifungashio vya plastiki, ikiwemo vya wasambazaji na vya chakula.
3. Vifaa vya kubebea chakula vya matumizi mara moja, ikiwa ni pamoja na mirija, vijiko/uma, mifuko, na vifuko vidogo (*sachets*)

Cha kutia moyo, biashara nyingi za utalii Zanzibar tayari zinafanya kazi kupunguza taka za plastiki.

## AINA ZA PLASTIKI NA MBINU BORA ZA MATUMIZI

**1 PET**
POLYETHYLENE TEREPHTHALATE
**INAPATIKANA KATIKA:** Chupa za maji na vinywaji.
**MBINU BORA:** Ondoa taratibu. Badilisha na mifumo ya maji inayojazwa tena.

**2 HDPE**
HIGH-DENSITY POLYETHYLENE
**INAPATIKANA KATIKA:** Vyombo vya bidhaa za kusafishia, makopo ya kuhifadhia.
**MBINU BORA: Inafaa sana kwa matumizi ya mara kwa mara na inaweza kuchakatwa tena nchini.**

**3 PVC**
POLYVINYL CHLORIDE
**INAPATIKANA KATIKA:** Filamu ya kufungia chakula, vifungashio vinavyokunjika, baadhi ya vifaa vya sintetik.
**MBINU BORA:** Epuka na ondoa taratibu.

**4 LDPE**
LOW-DENSITY POLYETHYLENE
**INAPATIKANA KATIKA:** Mifuko ya plastiki, filamu za kufungia, laina, na vifungashio laini.
**MBINU BORA:** Ondoa taratibu. Badilisha na mbadala au plastic zinazoweza kutumika tena.

**5 PP**
POLYPROPYLENE
**INAPATIKANA KATIKA:** Vyombo vya kuhifadhia chakula, vifuniko vya chupa, visambazaji.
**MBINU BORA:** Tumia kwa uangalifu. Hakikisha mfumo sahihi wa urejeshaji.

**6 PS**
POLYSTYRENE
**INAPATIKANA KATIKA:** Maboksi ya kubebea chakula, vikombe, treya, na vifungashio.
**MBINU BORA:** Ondoa taratibu. Badilisha na mbadala zinazoweza kutumika tena.

**7 OTHER**
OTHER PLASTICS
**INAPATIKANA KATIKA:** Plastiki mchanganyiko na maalum.
**MBINU BORA:** Isipokuwa imethibitishwa wazi kuwa salama, epuka na ondoa taratibu.

## UNUNUZI KIJANI – MUONGOZO WA REJEA

### A. BIASHARA NDOGO ZA UTALII

*(Nyumba za kulala wageni, hoteli ndogo, migahawa, mikahawa, vituo vya kupiga mbizi na waandaaji wa safari za utalii)*

#### ORODHA YA KUZINGATIA

- ☐ Omba wasambazaji wa mazao mapya walete bidhaa kwenye kreti, vikapu au magunia yanayoweza kutumika tena badala ya mifuko ya plastiki.
- ☐ Omba wasambazaji wa maji watoe vyombo vinavyoweza kujazwa tena au chupa kubwa zaidi pale zinapopatikana.
- ☐ Nunua bidhaa za kusafishia katika vyombo vikubwa na uulize wasambazaji kuhusu uwezekano wa kujaza tena.
- ☐ Himiza wasambazaji wa chakula na vinywaji kupunguza vifungashio visivyo vya lazima na kukusanya kreti zinazoweza kutumika tena.
- ☐ Waunge mkono wasambazaji na mafundi wa ndani wanaotoa mbadala zinazoweza kutumika tena au zisizo na plastiki.
- ☐ Epuka kupokea vifungashio vya Styrofoam (povu).
- ☐ Jadili upunguzaji wa vifungashio na angalau wasambazaji wakuu watatu kila mwaka.

#### VIASHIRIA VYA MAFANIKIO YA HARAKA

- ✓ Bidhaa za kusafishia zimenunuliwa kwa wingi (kwa vifungashio vikubwa).
- ✓ Maji ya kunywa ya wafanyakazi hutolewa kupitia mifumo ya kujaza tena.
- ✓ Mazao mapya hupokelewa zaidi katika vyombo vinavyoweza kutumika tena.
- ✓ Hakuna Styrofoam inayoingia kwenye biashara.

SKANI HAPA KWA
ORODHA YA WASAMBAZAJI ENDELEVU

### B. BIASHARA ZA KATI NA KUBWA ZA UTALII

*(Hoteli, miji ya mapumziko na makundi ya hoteli)*

#### ORODHA YA KUZINGATIA

- ☐ Tambua wasambazaji wanaozalisha kiasi kikubwa zaidi cha taka za vifungashio na uweke kipaumbele cha kushirikiana nao.
- ☐ Waulize wasambazaji jinsi vifungashio vinavyoweza kuondolewa, kupunguzwa, au kubadilishwa na mifumo ya usafirishaji inayoweza kutumika tena.
- ☐ Hamasisha ununuzi wa jumla na mifumo ya kujaza tena kwa bidhaa za kusafishia, huduma za wageni na vyakula.
- ☐ Watake wasambazaji waepuke Styrofoam na kupunguza vifungashio vya ziada.
- ☐ Wahimize wasambazaji kutekeleza mipango ya kuchukua tena kreti, vyombo na vifaa vya vifungashio.
- ☐ Jumuisha mazingatio ya kupunguza vifungashio na kupunguza taka katika maamuzi ya ununuzi.
- ☐ Fanya majadiliano ya kila mwaka na wasambazaji wakuu kuhusu fursa za kupunguza taka za plastiki.
- ☐ Fanya kazi na wadau wa usimamizi wa taka na urejelezaji ili kuhakikisha vifaa vilivyonunuliwa vinaweza kurejeshwa ndani ya nchi inapowezekana.

#### VIASHIRIA VYA MAFANIKIO YA HARAKA

- ✓ Hakuna Styrofoam iliyokubaliwa kutoka kwa wasambazaji.
- ✓ Mpango wa ununuzi wa jumla umetekelezwa.
- ✓ Mfumo wa kutumia tena au kurejesha umeanzishwa na angalau msambazaji mmoja mkuu.
- ✓ Vigezo vya uendelevu vya msambazaji vimejumuishwa katika maamuzi ya ununuzi.
- ✓ Mkutano wa kila mwaka wa ushiriki wa wasambazaji umefanyika.

CHUMBE ISLAND CORAL PARK · COMMISSION FOR TOURISM ZANZIBAR · Blue Impact NETWORK · ProsperBlue healthy ocean, prosperous people · german cooperation DEUTSCHE ZUSAMMENARBEIT · Co-funded by the European Union · giz Deutsche Gesellschaft für Internationale Zusammenarbeit (GIZ) GmbH

Miongozo ya REDUCE ilitengenezwa na Mtandao wa Blue Impact, kitovu endelevu cha utalii Zanzibar, kwa ushirikiano na Hifadhi ya Matumbawe ya Kisiwa cha Chumbe na Tume ya Utalii ya Zanzibar, kwa usaidizi wa kifedha wa Umoja wa Ulaya na Wizara ya Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo ya Shirikisho la Ujerumani (BMZ) kupitia Mradi wa ProsperBlue/Stawi Bluu unaotekelezwa na Deutsche Gesellschaft für Internationale Zusammenarbeit (GIZ) GmbH nchini Tanzania. Yaliyomo katika chapisho hili hayawakilishi msimamo rasmi wa Umoja wa Ulaya, BMZ na GIZ.